

416,000 zaidi kupata maji safi Arusha

Na Veronica Mheta, Arusha

WANANCHI zaidi ya 416,000 wa Mkoa wa Arusha wanatarajia kunufaika na mradi mkubwa wa maji baada ya serikali kutoa zaidi ya Sh bilioni 476 ili kupanua huduma za maji.

Akizungumza jana mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Mrisho Gambo katika Kata ya Olasiti ambayo ni miongoni mwa wanufaika na mradi huo wa miaka mitatu, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Taka Mkoa wa Arusha (AUWSA), Ruth Koya alisema mradi huo unatarajia kuanza Septemba mwaka huu na sasa wapo katika kukamilisha taratibu chache ili uanze.

Alisema mradi huo unatarajia kuzalisha maji lita milioni 200 kwa siku ambayo yatakidhi mahitaji ya wakazi wa Arusha kwa asilimia 100, kwani kwa sasa wanazalisha lita milioni 60 kwa siku ambazo hazikidhi mahitaji, lakini kwa kupata fedha hizo zitawawezesha kufanya shida ya maji historia kwa Arusha.

Aidha, alisema wanakabiliwa na changamoto ya wizi wa maji unaodaiwa kufanywa na baadhi ya hoteli kubwa na pia upotevu unaoitokana na uharibifu wa mambo wakati wa kutengeneza barabara.

Aidha, alisema wakazi wa Olasiti ambao wamekuwa miongoni mwa wananchi wenye shida kubwa ya maji, miezi michache ijayo watapelekewa bomba kubwa litakalotokea Magereza ambako kuna maji mengi na kupelekewa katika eneo lao.

Wavamizi shamba la mwekezaji watimuliwa

Na Mwandishi Wetu, Tarime

MKUU wa Wilaya ya Tarime, Glorious Luoga amewaagiza wenyeviti wa vijiji vya Murito na Gibaso wilayani hapa kuhakikisha wanasimamia kuondolewa haraka wananchi zaidi ya 200 waliovamia shamba la mwekezaji wa kilimo cha alizeti lenye ukubwa wa ekari 800 katika mpaka unaotenganisha vijiji hivyo.

Wananchi hao wanadai mwekezaji huyo hakutumiza masharti ya

Makandarasi miradi ya umeme waonywa

Na Mwandishi Maalumu, Njombe

SERIKALI imewataka makandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme nchini kuachana na visingizio vya uchelewaji wa fedha na badala yake watumie fedha zao kukamilisha miradi hiyo kwa wakati.

Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Dk Medard Kalemani aliyasema hayo hivi karibuni mkoani Njombe akiwa katika ziara kukagua utekelezaji wa miradi

mbalimbali ya umeme.

Alisema baadhi ya makandarasi wamekuwa na tabia ya kuchelewesha miradi wanayoismamia kwa kisingizio cha kutopokea fedha kutoka kwa wafadhili na hivyo aliwataka kuachana na tabia hiyo mara moja.


Alisema mojawapo ya sifa katika kuchagua mkandarasi ni pamoja na uwezo wake wa kifedha katika kutekeleza mradi husika, hivyo hakuna sababu ya mkandarasi kuchelewesha kazi kwa kisingizio cha fedha.

"Serikali haitavumilia wakandarasi wanaosuasua katika utekelezaji wa miradi wanayoismamia kwa kisingizio cha fedha. Fedha kutoka kwa wafadhili inapochelewa, wao watumie fedha zao kwani uhakika wa kulipwa upo," alisisitiza.

Akizungumza baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa Makambako - Songea, Dk Kalemani aliwataka maofisa wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) wanaosimamia miradi mbalimbali ya umeme nchini kuhakikisha wanawasi-

mamia makandarasi ipasavyo ili kukamilisha miradi kwa wakati na kwa viwango.

Alisema Mradi wa Makambako - Songea ni mojawapo ya miradi muhimu kwa Taifa hususan kwa wananchi wa maeneo husika, hivyo ni lazima ukamilike kwa wakati uliopangwa ambao siyo zaidi ya mapema mwaka 2018. Alisema matarajio ya serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025, vijiji vyote vya Tanzania vinakuwa na umeme hivyo ni lazima kufanya kazi kwa bidii ili kufikia malengo hayo.



Rais mstaafu Jakaya Kikwete akifungua mkutano wa 3 wa Sera za Mabadiliko ya Tabia Nchi ulioandaliwa na Taasisi ya Uongozi kwa kushirikiana na Climate Strategies, Dar es Salaam juzi. Kutoka kulia ni Mwenyekiti wa mkutano huo, Chuks Okereke, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), January Makamba na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, Profesa Joseph Semboja. (Na Mpigapicha Wetu).

DC Meatu akemea kazi kwa mazoea

Na Karen Masasy, Meatu

MKUU wa Wilaya ya Meatu mkoani Simiyu, Joseph Chilangani amewaonya baadhi

kazi kwa mazoea na wasome alama za nyakati kwa kuzingatia nidhamu, uadilifu, haki, sheria na kuepuka rushwa ili kuharakisha maendeleo ya wananchi.

Aliwaonya watendaji hao juzi

mjini Mwanhuji, wakati wa kujibu hoja za Mdhidhi wa Hesabu za Serikali (CAG) kutokana na halimashauri hiyo kupata hati yenye mashaka.

Alisema wanapaswa kuepuka

ghulikia kero ili kila mmoja ajione ana haki sawa na kwamba kila kiongozi katika eneo lake la kazi sharti azingatie haki, nidhamu, uadilifu na kuepuka rushwa ili kuleta maendeleo ya wananchi kwa